

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu: +255 262 963309/13/14

Nukushi: +255 262 963 316

Barua pepe: km@ardhi.go.tz

Tovuti: www.ardhi.go.tz



1 Mtaa wa Ardhi,

S. L. P. 9132,

11477 DAR ES SALAAM.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CA.174/333/04.I/17

11 Agosti, 2022

Mkurugenzi wa Manispaa,

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke,

92 Barabara ya Nelson Mandela,

S.L.P 46343,

15883 - DAR ES SALAAM.

**YAH: MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI YA ARDHI YA VIWANJA NA
464, 465, 466, 467, 468, 469, 470 NA 471 KITALU 'C' KIJICHI KUTOKA MAKAZI
PEKEE KUWA KIWANDA CHEPESI NA GHALA.**

Tafadhali rejea barua yako yenye Kumb. Na. TMC/LD/KBM/VOL.XI/79 ya tarehe 28 Machi, 2022 kuhusiana na somo tajwa hapo juu. Maombi tajwa ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliridhiwa na Kikao cha Kamati ya Mipangomiji cha Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kilichofanyika tarehe 24/12/2021.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 kifungu cha 6(3) (k) napenda kukujulisha kuwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi ameridhia na kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi ya Viwanja Na.464, 465, 466, 467, 468, 469, 470 na 471 Kitalu 'C' Kijichi Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kutoka makazi na biashara kuwa kiwanda chepesi na Ghala. Masharti mapya ya uendelezaji yatazingatia Kifungu 'M' kijifungu (a), (b), (c), (d) na (e) na Kifungu 'L' kama ilivyobainishwa katika Sheria ya Mipangomiji Na 8 ya 2007 Kifungu cha 77 (1) (i) (Kanuni ya vifungu vya matumizi) ya GN 91 na 93 za tarehe 09/03/2018.

Masharti maalum yatakayopaswa kuzingatiwa kwenye mabadiliko hayo ya matumizi ya ardhi ni yafuatayo:-

1. Kuwasilisha Nyaraka za Hatimiliki kwa Halmashauri ya Manispaa ya Temke ili kukamilisha taratibu za mabadiliko ya matumizi ya ardhi (*variation*).
2. Kupata kibali cha ujenzi hutoka Halmashauri ya Manispaa ya Temke kabla ya kuanza ujenzi;
3. Kujenga majengo mawili ya kawaida ya mfuto, kwa kuzingatia uwiano wa (*plot ratio*) 1.2 na ujazo (*plot coverage*) wa asilimia 60, 'setback' umbali wa mita 15 kw mbele, upande mita 3 na nyuma mita 5.
4. Kuimarisha mfumo wa maji safi na maji taka katika kiwanja (wawasiliane na DAWASA);
5. Kuweka mfumo thabiti wa kudhibiti moto (wawasiliane na Kikosi cha Zimamoto kabla ya kuanza ujenzi);
6. Ujenzi na matumizi ya viwanja usiathiri mazingira na matumizi ya ardhi ya viwanja jirani;
7. Ujenzi uzingatie kuwepo kwa magesho ya magari malano (5) kwa kila mita za mraba 1000 za ujenzi.

Nashukuru kwa ushirikiano.



M. Bahitwa

Kny: KATIBU MKUU

Nakala:

Kamishina Msaidizi wa Ardhi,
Kanda ya Dar es Salaam,
S.L.P 9132,
DAR ES SALAAM. (Tafadhali badilisha kiwango cha kodi)

Mohamed Rafique Daud, Abdallah Ayaz Mohamed na Rafique Daud Abdallah
S.L.P 5804,
DAR ES SALAAM. (Kwa taarifa)